



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.HW/KOG/F.20/2.VOL VII/133

24 Septemba, 2024

TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA ZA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa ya kuomba nafasi ya Ajira ya Mkataba ya **Wakusanya Mapato**.

1.1 Sifa za Mwombaji:

Mwombaji anatakiwa awe ni mwenye Elimu ya Kidato **cha Nne/Sita** au aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti.

1.2 Sifa za ziada;

Mwombaji ambae amefuzu mafunzo ya Jeshi la Akiba (Mgambo) atafikiriwa zaidi. Na asiwe amewahi kufanya kazi hii hapo awali.

1.3 Kazi/Majukumu ya Mkusanya Mapato:

- ❖ Kukusanya Ushuru eneo lote linalokuzunguka kwa kutumia Mashine ya Posi.
- ❖ Kukata au kutoa Risiti.
- ❖ Kuhakikisha unadhibiti utoroshwaji wa Mazao na Mapato ya vyanzo Vyote katika eneo la ukusanyaji.
- ❖ Kuhakikisha kila chanzo kinachopaswa kulipa Ushuru kinalipa.
- ❖ Kushirikiana na Mtendaji wa Kata/ Kijiji katika kukusanya Ushuru.
- ❖ Kukagua kila Gari au Mzigo unaopita kwenye eneo la ukusanyaji.
- ❖ Kuriporti mara moja kwa Mhasibu au Wasaidizi wake punde tu unapopata changamoto.
- ❖ Kupeleka Benk Fedha zote za Makusanyo ya Mapato kwa wakati.

MASHARTI YA JUMLA:

- ❖ Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye Umri kati ya Miaka 20 hadi 35.
- ❖ Waombaji waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza Curriculum Vitae (CV) yenye Anuani inayotumika, Namba za Simu na **Anuani ya barua pepe** (E-mail adres) pamoja na majina ya Wadhamini (**Referees**) watatu wa kuaminika.
- ❖ Waombaji wote waambatishe Cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
- ❖ Mwombaji awe na namba ya kitambulisho cha Taifa /NIDA

- ❖ Maombi yote yaambatane na Vyeti vya Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni Vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na Vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- ❖ Uwasilishaji wa Taarifa na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.
- ❖ Barua ya Maombi iandikwe kwa Kiswahili.
- ❖ Mwisho wa kupokea barua za maombi ni **Septemba 30,2024** siku ya Jumatatu.
- ❖ Mwombaji awasilishe Picha moja ya hivi karibuni (Passport Size).
- ❖ Maombi yote ya kazi yapitie kwa Mtendaji wa kata kasha yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji.
- ❖ Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika Tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA**
- ❖ **Muhimu:** kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na Vyeti ya Elimu, aidha, Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA,
S.L.P 57,
KONGWA – DODOMA.**

Imetolewa na :



.....
Dr. Omary A. Nkullo
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KONGWA**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA
S. L. P.
KONGWA**